



# MEDICAL COUNCIL OF TANGANYIKA

Guiding the profession, Protecting the public  
(Communications to be addressed to THE REGISTRAR)

OFFICE OF REGISTRAR,  
P.O. BOX. 743 DODOMA.  
Phone: +255656931365  
Email: info@mct.go.tz

## **TAARIFA KWA UMMA NA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU MASHAURI KUMI NA MOJA YA KITAALUMA YALIYOWASILISHWA MBELE YA BARAZA LA MADAKTARI TANGANYIKA**

Ndugu wananchi na vyombo vya habari.

Baraza la Madaktari Tanganyika limeundwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Udaktari, Udaktari wa Meno na Afya Shirikishi Sura namba 152 ya mwaka 2017. Miongoni mwa majukumu ya Baraza ni pamoja na kusimamia maadili ya wanataaluma ya Udaktari, Udaaktari wa Meno na Afya Shirikishi lakini pia kufanya uchunguzi kwa kutumia kamati yake ya uchunguzi na kuendesha mashauri ya kitaaluma kadri yanavyowasilishwa mbele ya Baraza kwa lengo la kutoa haki kwa pande zote mbili yaani mlalamikaji na mlalamikiwa ambaye anaweza kuwa daktari, daktari wa meno au mtaalamu wa afya shirikishi mfano mifiziotherapia.

Aidha, Baraza la Madaktari Tanganyika lina mamlaka chini ya kifungu cha 42(1-2) cha Sheria ya Udaktari, Udaktari wa Meno na Afya Shirikishi endapo litaona kuna shauri la kujibu, ya kumuita mlalamikiwa na baada ya utaratibu mzima wakusikiliza shauri husika kukamilika na kama mlalamikiwa atakutwa na hatia, litatoa adhabu ya onyo, onyo kali, kusitisha kutoa huduma kwa muda, kufutwa kwenye daftari la usajili au kuamuru mlalamikiwa kulipa gharama za uendeshaji wa shauri husika kama ilivyo chini ya kifungu cha 42(4)(a-d) cha sheria hiyo.

Katika muendelezo wa kutekeleza jukumu hili la usikilizaji wa mashauri, Baraza la Madaktari Tanganyika lilikaa Jijini Dar es salaam kuanzia tarehe 20 hadi 27 Septemba 2021 kwa ajili ya kusikiliza mashauri mbalimbali kama yalivyowasilishwa na hivyo

kuona ni busara kutoa taarifa kwa umma kwa lengo la kuwafahamisha baadhi ya mambo yaliyojitokeza wakati wa kusikiliza mashauri hayo.

Baraza limesikiliza jumla ya mashauri kumi na moja (11) ambapo kati ya haya mashauri sita (6) ni Magonjwa ya Wanawake na uzazi ( Obstetrics & Gynaecology), matatu (3) ni ya upasuaji na mashauri mawili (2) ni ya kukiuka kanuni za maadili na utendaji wa kitaaluma.

Baada ya kusikiliza mashauri yote kumi na moja(11), Baraza limetoa hukumu zifuatazo dhidi ya wanataaluma:-

- i. Dr. Mlindwa Yahaya Mazana- Kafutwa kwenye daftari la Usajili
- ii. Dr. Joel Chunga – Kasitishwa kutoa huduma kwa miezi sita
- iii. Dr. Joshua Garrison- Hajakutwa na hatia
- iv. Dr. Antidius Mchunguzi – Hajakutwa na hatia
- v. Dr. Najma Awadh – Kusitishwa kutoa huduma kwa miezi mitatu.
- vi. Dr. Leader Kamonjo – Amepewa Onyo
- vii. Dr. Milton Kabilingi – Amepewa Onyo
- viii. Dr. Tumai Tumaini Baumba = Hajakutwa na hatia
- ix. Dr. Josephat Mponji – Amepewa Onyo kali

Aidha, mashauri mawili (2) yameahirishwa kutokana na wahusika kushindwa kufika kwa sababu zilizowasilishwa mbele ya Baraza.

Pande zote mbili zimefahamishwa haki ya kukataa rufaa kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 43(2),(3) na 44 cha sheria ya Udaktari, Udaktari wa Meno na Afya Shirikishi.

Baraza linatoa wito kwa wanataaluma kuzingatia Kanuni na maadili ya kitaaluma za mwaka 2005 na kufuata miongozo ya utoaji huduma haswa katika ujazaji wa fomu za ridhaa ya huduma (informed Consent) lakini pia kuwafahamisha wagonjwa changamoto kama zipo, zinazoweza kusababishwa na huduma mbalimbali wanazowapa.

Baraza la Madaktari Tanganyika linapenda pia kuufahamisha umma wa watazania kuwa halina mamlaka ya kisheria ya **KUTOA FIDIA** kwa mlalamikaji au mlalamikiwa kwani mamlaka hii ipo chini ya mahakama.

Imetolewa leo tarehe 24/09/2021



Prof. David Ngassapa

**MWENYEKITI  
BARAZA LA MADAKTARI TANGANYIKA**